# M I S A
# YA MTAKATIFU BONIFACIA RODRIGUEZ DE CASTRO
# BIKIRA

*Ant.* *Zab. 36,3-4*

Umtumaine Bwana na kutenda mema, ili ukae katika nchi, ule chakula kwa salama, uwe na furaha yako katika Bwana, naye atakujalia maombi ya moyo wako.

*SIFA inaimbwa*

*SALA ya mwanzo*

Ee Mungu, Baba yetu,
ulimwita mwenyi heri Bonifacia, Bikira,
amfuate Mwana wako katika maisha yake ya Nazarethi,
na tena awatumikie maskini, akiunganisha sala na kazi;
tunakuomba:
sisi, vile kama yeye, tutafute Ufalme wako katika mambo yote,
na tufurahiwesiku mja, katika nyumba yako, na mema ya umilele.
Kwa ajili ya Bwana wetu Yesu Kristu, anayeishi na kutawala
pamoja nawe, milele na milele.

*Kuna "Sala ua kusadiki"*

*SALA ya matoleo*

Tunakutolea leo na furaha sadaka takatifu, ee Bwana, tunamokumbuka ushindi tukufu wa Mtakatifu Bonifacia. Pamoja naye tunatangaza ukubwa wako na tunakuwa na furaha kubwa kwa sababu umetujalia maombezi yake. Kwa ajili ya Kristu, Bwana wetu.

*Ant. Kisha komunyo* *Yo. 12,26*

Mtu akitaka kunitumikia, anifuate, asema Bwana; na pale nilipo, mtumishi wangu pia atakuwapo.

*SALA kisha komunyo*

Ee Baba Mungu, tunakuomba: Eklezya yako ipewe ukamilifu na wokovu ndani ya sakramenta hiyo, tunamolishwa tukimshangilia Mtakatifu Bonifacia. Yeye aliyekuwa sifa ya Eklezya yako alipowatumikia maskini, awe sasa mlinzi wetu mbinguni. Kwa ajili ya Yesu Kristu, Bwana wetu.

*MASOMO Wakati wa Paska*

*SOMO la kwanza Matendo 2,42-47 "Waamini wote walikuwa shirika moja na vitu vyao vyote wakavitia kusharikiwa na wote."*

Nao walikuwa wakidumu imara katika mafundisho ya Mitume, na ushirika wa kindugu, katika kumega mkate na kusali. Hofu ikawaingia watu wote, maana maajabu na ishara nyingi zilifanyika kwa nguvu ya Mitume. Waamini wote walikuwa shirika moja, na vitu vyao vyote wakavitia kusharikiwa na wote. Wakauza mashamba yao na vitu walivyokuwa navyo, wakavigawanya kwa wote, kadiri ya mahitaji ya kila mmoja. Siku kwa siku walikwenda hekaluni kwa imara na kwa moyo mmoja. Tena, wakimega mkate katika nyumba, walikula pamoja kwa furaha na moyo mnyofu, wakimsifu Mungu na kuwapendeza watu wote. Na siku kwa siku Bwana akaliongezea shirika lao watu wenye kuokoka.

*ZABURI 117,2-4. 13. 15. 22-24*

*R/ Zab. 117,1*

Mshukuruni Bwana kwani ndiye mwema,
kwani wema wake ndio wa milele.

Israeli na aseme:
kweli wema wake ndio wa milele.
Nyumba ya Aroni iseme
kweli wema wake ndio wa milele.
Wenye kumwabudu Bwana waseme:
kweli wema wake ndio wa milele.

*R/* Mshukuruni Bwana …

Nilisukumwa, nilisukumizwa nianguke,
lakini Bwana amenisaidia.
Sauti ya shangwe na ya ushindi
imo katika hema za watu wema:
mkono wa kuume wa Bwana umetenda makuu.
*R/* Mshukuruni Bwana …

Jiwe walilokataa wajengaji
limekuwa jiwe la pembe:
ndilo jambo alilofanya Bwana,
nasi twaliona ni ajabu.
*R/* Mshukuruni Bwana …

Hii ndiyo siku aliyofanya Bwana,
tushangilie na kufurahiwa nayo.
*R/* Mshukuruni Bwana …

*MASOMO*
*Katika Mwaka*

*SOMO la kwanza Yesaya 42,1-4.6-7*
*"Huyu ndiye mtumishi wangu ninayemtegemeza."*

Huyu ndiye mtumishi wangu ninayemtegemeza,
mteule wangu, moyo wangu unapendezwa naye.
Nimeweka roho yangu juu yake.
Atawajulisha mataifu hukumu.
Hatalia wala kupaliza sauti:
wala hatafanya kelele katika njia za mji.
Hatalivunja tete lililokunjika, hatakomesha utambi unaozimika;
bali atajulisha hukumu kwa ukweli.
Hatazimia wala hatakunjika, mpaka atakapoweka hukumu duniani,
na visiwa vintagonjea mafundisho yake.

Mimi Bwana, nimekuita kwa ajili ya haki,
nimekushika mkono, nimekuumba nikakuweka kuwa agano la taifa
na mwangaza wa mataifa.
Ili kuwafumbua vipofu macho, ili kuwaondosha vifungoni waliofungwa
na gerezani wale wanaokaa gizani.

*ZABURI 117 (kama hapa juu)*
*R/ " Umsifu Mungu kwani ni mwema, kwani huruma yake ni ya milele!"*
*Ao:* Aleluya

*SOMO la pili Wafilipi 2,1-11*

Je, mnataka kweli kuleta kitulizo katika Kristu, na kuwaita wengine katika mapendo? Je, kama mnataka kusharikiana katika Roho, na kuonyesha moyo mwema na wenye huruma? Basi ikamilisheni furaha yangu kwa kuwaza mamoja, kwa kupenda mamoja, kwa kuwa na roho moja, kwa kushurulikia umoja. Wala ushindani wala majivuno ya bure visipatikane kati yenu; lakini kwa unyenyekevu mwawazie wengine kuwapita ninyi wenyewe. Kila mmoja wenu asiangalie yaliyo yake tu, bali yaliyo ya wengine pia. Muwe kati yenu na mawazo yale aliyokuwa nayo Kristu Yesu.

Yeye, aliye na hali ya Mungu,
hakutaka kushikamana kabisa
na cheo chake cha kuwa sawa na Mungu.

Bali aliachila hicho
akatwaa hali ya mtumwa,
na kugeuka sawa na wanadamu,

Akaonekana mwenye umbo la mtu,
akajinyenyekeza, akawa mtii mpaka kufa,
hata kufa mslabani.

Kwa hiyo Mungu alimtukuza sana,
akamjalia Jina,
lenye kupita jina lolote:

ili kwa jina la Yesu
wote wapige magoti,
walio mbinguni, duniani na kuzimuni;

Na kila ulimi uungame
ya kwamba Yesu Kristu ndiye Bwana
kwa utukufu wa Mungu Baba.

*ALELUYA Yesaya 61,1*

Aleluya, Aleluya.
Roho ya Bwana yupo juu yangu.
Amenituma niwahubiri maskini habari njema.
Aleluya.

*ENJILI Lk. 4,16-24 "Roho ya Bwana juu yangu, kwani amenipaka mafuta."*

Yesu akafika Nazareti, ndipo alipokulia; akaingia katika sinagogi siku ya sabato, kama alivyozoea. Akasimama awasomee watu. Akapewa kitabu cha nabii Yesaya, akakunjua kitabu, akakuta mahali penye kuandikwa:

"Roho ya Bwana juu yangu
kwa sababu amenipaka mafuta.
Amenituma niwahubiri maskini Habari Njema,
kuwaponya waliovunjika moyo,
kuwatangazia waliotekwa kufunguliwa kwao, na vipofu kuona tena;
kuwaletea walioelemezwa uhuru, kutangaza mwaka wa rehema ya Bwana."

Yesu akakunja kitabu, akamrudishia mtumishi, akaketi. Nao wote waliokuwamo katika sinagogi, walikuwa wakimtazamia macho. Akaanza kuwaambia: "Leo limetimia Andiko hili mlilosikia." Wote wakamkubalia, wakashangaa kwa maneno yenye neema yaliyotoka kinywani mwake. Wakasema: "Je, huyu si mwana wa Yosefu?" Akawaambia: "Bila shaka mtaniambia mfano huu: 'Mganga ujiponye mwenyewe!' Yale mambo makubwa tuliyosikia kwamba yametendeka Kafarnaumu, uyatende pia hapa mjini mwako." Akasema: "Nawaambieni kweli: Hakuna nabii hata mmoja mwenye kupokewa katika mji wake mwenyewe."

6 Yuni

# Mtakatifu Bonifacia Rodriguez de Castro, Bikira

SIKU KUU

Bonifacia Rodríguez Castro amezaliwa Salamanque (España) tarehe 6 juni 1837, katika jamaa ya watenda kazi . Ameanza kutumika katika ufundi wa kushona tangu umri wa miaka 15. Alikuwa na ibada kubwa kwa Mtakatifu Yusufu na kwa Maria asiye na zambi. Alianzisha shirika la “JOSEPHINE” pamoja na rafiki zake katika nyumba yake ya ufundi. Akisaidiwa na Padri Francisco Butiyná, Jesuiti wa Catalani, anaanzisha mgini wa Salamanca, mwaka 1874, Shirika la “Watumishi wa Mtakatifu Yusufu” na nia ya kuwakinga wamama watenda kazi maskini. Kwa maisha ya kiroho anashindilia hasa: Umoja kati ya sala na kazi katika maisha ya kila siku, kwa kuiga hivi mfano wa jamaa ya Nazarethi. Katika maisha yake anapata majaribu ya kutengwa, kushushwa na kusingiziwa uwongo. Jibu lake ilikuwa moja tu: ukimya na msamaha, yenye kuonyesha wazi mapendo yake ya kindugu. Anafariki mgini Zamora (España) taree 8 augusto, 1905.

## 1. Sala ya kwanza ya mangaribi.

*WIMBO*

*Ant. 1* Jina la Bwana litukuzwe, aliyenitendea maajabu. *(W.P. :* Aleluya)

*ZABURI 112*

Enyi watumisha wa Bwana, sifuni, lisifuni jina la Bwana.
Jina la Bwana litukuzwe tangu sasa na hata milele.
Tangu kupanda kwa jua mpaka kushuka kwake jina la Bwana lisifiwe !

Bwana ni mkuu juu ya mataifa yote, utukufu wake ni juu ya mbingu.
Nani aliye sawa na Bwana, Mungu wetu, anayekaa juu kabisa,
anayeinama atazame chini yaliyomo mbinguni na duniani ?

amweke pamoja na wakubwa, pamoja na wakubwa wa taifa lake ;
amkalisha nyumbani mwanamke aliye tasa, awe mama mwenyi kufurahiwa na watoto.

*Ant.* Jina la Bwana litukuzwe, aliyenitendea maajabu. (*W.P. :* Aleluya)

*Ant. 2* Umsifu Bwana aliyekusindikiza kama Baba katika njia zako. *(WP. :* Aleluya)

*ZABURI 147*

Umtukuze Bwana, ee Yerusalemu, umsifu Mungu wako, ee Sioni.
Kwani amekaza makomeo ya milango yako, amewabariki wana wako ndani yako.
Ameweka amani katika mipaka yako, anakushibisha kwa unono wa ngano.

Anapeleka neno lake duniani, neno lake linapiga mbio sana.
Anatoa seluji kama vile pamba, anatapanya umande kama majivu.

Anatupa barafu yake kama mvua ya mawe, nani anayevumilia ubaridi wake ?
Anatoa amri yake, anaviyeyusha, anavumisha upepo wake, maji yanatiririka.

Amempasha Yakobo neno lake, Israeli amri na kanuni zake.
Hakuna taifa lingine alilotendea hivyo; wala hawakufumbulia kanuni zake.

*Ant.* Umsifu Bwana aliyekusindikiza kama Baba katika njia zako. *(W.P. :* Aleluya)

*Ant. 3* Asifiwe Mungu aliyekuchagua katika Kristu, ili uwe mtakatifu na bila kosa
mbele yake kwa ajili ya mapendo. *(W.P. :* Aleluya)

*WIMBO Waefeso 1,3-10*

Atukuzwe Mungu baba wa Bwana wetu Yesu Kristu,

aliyetubariki mbinguni katika Kristu, kwa baraka yoyote rohoni.

Kwani ametuchagua ndani yake Yeye, ulimwengu ulipokuwa haujasimikwa bado,
ili tuwe watakatifu na watu wasio na kosa mbele ya macho yake.

Kwa mapendo yake ametuweka tangu mwanzo
tumepokelewa naye kuwa wana wake kwa njia ya Kristu, na ndani yake.

Amekusudia hivyo katika mapenzi yake mema,
apate kusifiwa utukufu wa neema yake, aliyotujalia katika Mwana wake mpenzi.

Katika damu yake huyo tumepewa ukombozi,
na maondoleo ya makosa yetu, kadiri ya wingi wa neema yake.

Mungu amezidisha ndani yetu neema hiyo, inayotuletea hekima na ufahamu wote,
maana ametujulisha Fumbo la wokovu, alilokusudia katika mapenzi yake mema.

Katika Mwana wake ameweka tangu mwanzo Fumbo hilo,
apate kulitimiza nyakati zinapotimia: kukusanya vyote chini ya kichwa kimoja,
ndiye Kristu, vyote vya mbinguni na vyote vya duniani.

*Ant.* Asifiwe Mungu aliyekuchagua katika Kristu, ili uwe mtakatifu na bila kosa
Mbele yake kwa ajili ya mapendo. *(W.P.:* Aleluya)

*SOMO FUPI Wafilipi 3,7-8*

Lakini yaliyokuwa faida kwangu, niliyaona kuwa upotevu kwa ajili ya Kristu. Na kweli, ninaona mambo yote ni upotevu, nikiyafananisha na faida kuu ya kumjua Kristu Yesu Bwana wangu. Kwa ajili yake Yeye, nimependa kupotewa na yote nikiyaangalia kama takataka, ili nimpate Kristu.

*KIITIKIO*

*Mwakani*

*R/* Mali yangu ni Mungu milele: * Bwana ni mwema kwa yule anayemgeukia.
*V/* Katika ukimya ninangojea msaada wake. * Bwana…
Sifa kwa Baba… *R/* Mali yangu…

*Wakati wa Paska*

*R/* Mali yangu ni Mungu milele : Bwana ni mwema kwa yule anayemgeukia.
* Aleluya, Aleluya.
*V/* Katika ukimya ninangojea msaada wake. * Aleluya, Aleluya.
Sifa kwa Baba… *R/* Mali yangu…

*MOYO WANGU (Wimbo wa Bikira Maria Lk. 1,47-55)*

*Ant.* Bonifacia mwanamke wa kazi, anajitolea kwa kuwatumikia wanawake wafanya kazi wengine, akawarudishia heshima yao, na kuwapenda na kuwatunza kama kiini cha jicho lake. (*W.P.:* Aleluya)

- Moyo wangu unamtukuza Bwana,
na roho yangu inamshangilia Mungu, mwokozi wangu:
- Maana ameangalia udogo wa mtumishi wake,
kweli tangu leo vizazi vyote vitanitaja mwenyi heri,
- kwani Mwenyezi amenitendea makuu:
Jina lake ni takatifu.
- Wema wake umeenea vizazi kwa vizazi,
kwa watu wenyi kumheshimu.
- Ametenda nguvu kwa mkono wake
amewatawanya wenyi kujivuna moyoni.
- Amewaangusha wakubwa chini ya viti vya ezi,
amawapandisha wadogo.

- Wenyi njaa amewajaza mali;
wenyi mali amewaondosha mikono mitupu.
- Amemeshurulikia Israeli mtumishi wake,
Akikumbuka wema na ahadi zake,
- alizozitoa kwa baba zetu
Abrahamu na wazao wake kwa umilele.

*Ant.* Bonifacia mwanamke wa kazi, anajitolea …

*MAOMBI*

- Tunamshukuru Mungu kwa majitoleo ya Mtakatifu Bonifacia kwa ajili ya wamaskini na tunasema: wafurahi wale wote wanaotumainia kwako, ee Bwana.
- Tunakushukuru, ee Bwana, kwa mapendo yako kwa ajili yetu, ambayo yanatualika tuungane nawe kwa kujenga Ufalme wako.
- Utufanye tuwe chumvi na mwanga katika Eklezya yako, ili wale wanaotutazama wamsifu Baba yetu aliye mbinguni.
- Tunakushukuru, ee Baba, kwani unazidi kuwaita watu waingie katika maisha ya kitawa, ili, wakimfuata Yesu, wawasaidie watu kupokeleana, kuheshimiana na kusaidiana na hivyo watangaze Ufalme wako.
- Utusadie tuendeleshe kati ya wamaskini wafanya kazi, na hasa kati ya wamama, habari njema, kama vile ulivyomwalika Mtakatifu Bonifacia.
- Wewe unawapokea katika mapendo yako ndugu zetu waliofariki na unatualika tulinde umoja na undugu pamoja nao na pamoja na watakatifu wote.

Baba yetu…

*SALA*

Ee Mungu Baba yetu, ulimwita takatifu Bonifacia, bikira, amfuate Mwana wako katika ukimya na kuwatumikia maskini katika sala na kazi, utujalie kwa mfano wake, tutafute Ufalme wako kuliko vitu vyote hapa duniani na tusharikie mema ya milele ndani ya nyumba yako. Kwa ajili ya Kristu Yesu, Bwana wetu. Amina.

## 2. ZABURI YA MAALIKO.

*V/* Bwana ufungue midomo yangu.

*R/* Na kinywa changu kitatangaza sifa yako.

*Ant.* Tumsifu Bwana tunapomshangilia Mtakatifu Bonifacia. *(W.P.:* Aleluya)

*ZABURI 94 (ao mazaburi 99, 66, 24)*

Njoni! Tumpigie Bwana kelele za furaha,
tumshangilie Mwamba wa wokovu wetu;
tuje mbele yake kwa mashukuru,
tumshangilie kwa nyimbo na zaburi.

Kwani Bwana ni Mungu mkuu,
ni Mfalme mkuu juu ya miungu wote.
Mabonde ya dunia yamo mikononi mwake,
na vilele vya milima ni mali yake.
Bahari ni yake, maana Yeye ameifanya ;
Nayo nchi kavu, mikono yake imeiumba.

Njoni, tumwinamie na kumwangukia,
tumpigie magoti Bwana aliyetuumba !
Kwani Yeye ni Mungu wetu,
sisi lakini ni watu wa malisho yake,
na kondoo wanaochungwa na mkono wake.

Heri ninyi mukisikia sauti yake!
Msifanye mioyo yenu kuwa migumu kama huko Meriba,
Kama baba zenu walivyokuwa siku ya Masa,
waliponijaribu, baba zenu waliponipima,
ijapo walikwisha ona matendo yangu.

Miaka makumi manne nilichukizwa na kizazi hicho,
nikasema: “Ni watu wenyi kupotoka moyoni,
wala hawakujua njia zangu.”

Basi nikaapa kwa hasira yangu:
“Hawataingia katika raha yangu!”

*WIMBO*

*Ant. 1* Na hekima anafungua kinywa, ulimi wake unafundisha uwema. *(W.P.:* Aleluya)

*ZABURI 18,2-7*

Mbingu zaeleza utukufu wa Mungu,
anga latangaza kazi ya mikono yake.
Mchana hupasha mchana habari,
nao usiku huujulisha usiku.

Hakuna neno, hakuna usemi,
wala sauti yake haisikiliki.
Lakini uvumi wake waenea duniani kote
na maneno yake hata mipaka ya ulimwengu.

Huko amelipigia jua hema yake,
nalo hutoka kama bwana arusi chumbani mwake,
hufurahiwa kama shujaa likipita njia kwa mbio.
Hutoka katika mpaka wa anga,
na kuzunguka hata mpaka wa anga,
wala hakuna chenye kuiepuka joto lake.

*Ant.* Na hekima anafungua kinywa chake, ulimi wake unafundisha uwema.
(*W.P.:* Aleluya)
*Ant. 2* Ulipenda uhaki, ndiyo sababu Bwana Mungu wako alikujalia na furaha.
*(W.P.:* Aleluya)

*ZABURI 44,2-10*

Moyo wangu unatoa neno bora:
namwambia mfalme wimbo wangu;
ulimi wangu ni kalamu ya mwandishi mwepesi.

Wewe ni mzuri kuliko wanadamu,
neema imemiminika midomoni mwako,
kwa hiyo Mungu amekubariki hata milele.

Ewe shujaa, weka pajani upanga wako;
ndio urembo wako na pambo lako.
nenda ukafanikiwe kuipigania uaminifu na haki,
na mkono wako wa kuume utende mambo ya sifa.

Mishale yako ni mikali; mataifa kuwekwa chini yako;
adui za mfalme wapungukiwa moyo.

Ee Mungu, kiti chako kipo milele na mille,
bakora ya ufalme wako ni bakora ya haki.

Wapenda haki, wachukia wovu,
ndiyo sababu Mungu, Mungu wako,
amekupaka mafuta ya furaha, kuliko wenzako.

Mavazi yako yanukia manemane, udi na dalasini;
vinubi vinakufurahisha toka majumbe ya pembe.
Mabinti wa wafalme kati ya wapenzi wako,
malkia amesimama mkono wako wa kuume,
amevaa mapambo ya zahabu ya Ofiri.

*Ant.* Ulipenda haki, ndiyo sababu Bwana Mungu wako alikujalia na furaha.
*(W.P.:* Aleluya)

*Ant. 3* Nataka kukumbusha jina lako kizazi kwa kizazi na mataifa yote
Watakutukuza milele na milele. *(W.P.:* Aleluya)

*ZABURI 44,11-18*

Sikia ee binti, utazame, utege sikio lako,
usahau kabila lako na nyumba ya baba yako.
Naye mfalme atatamani uzuri wako,
maana yeye ni bwana wako, umwangukie.
Watu wa Tiro wanakuja wenye zawadi,
matajiri wa kabila watazamia upendeleo wako.

Binti mfalme anaingia akivikwa vizuri ajabu,
vazi lake ni la mfumo wa zahabu.
Analetwa kwa mfalme akivaa vazi la rangi nyingi ;
nyuma yake, mabinti wenzake wanapelekwa kwako.
Wanaletwa kwa furaha na kelele za shangwe,
wanaingia katika jumba la mfalme.

Mahali pa baba zako watakuwapo wana;
utawafanya kuwa wakuu katika dunia nzima.
Nitalitangaza jina lako kizazi kwa kizazi;
kwa hiyo mataifa watakutukuza milele na milele.

*Ant.* Nataka kukumbusha jina lako kizazi kwa kizazi na mataifa yote
Watakutukuza milele na milele. *(W.P.:* Aleluya)

*V/* Upokee maneno ya kinywa changu. *(W.P.:* Aleluya)
*R/* Bwana ndiwe mwamba wangu na kimbilio langu. *(W.P.:* Aleluya)

*SOMO la kwanza 1 Yoane 4,7-21*

Wapenzi wangu: tupendane, kwani mapendo yatoka kwa Mungu, na kila mtu anayependa amezaliwa na Mungu, naye amjua Mungu. Asiyependa hakumtambua Mungu, kwani Mungu ni mapendo. Katika jambo hilo mapendo ya Mungu yameonekana

waziwazi, ya kuwa Mungu alimtuma Mwanae wa pekee duniani, ili tuwe na uzima kwa njia yake. Mapendo hayo ndivyo yalivyo: sio sisi tuliompenda Mungu, bali ni Yeye aliyetupenda sisi, akamtuma Mwanae awe sadaka ya malipo kwa ajili ya zambi zetu. Wapenzi wangu: kama Mungu alitupenda sisi vile, nasi tunapaswa kupendana. Hakuna mtu aliyemwona Mungu hata mara moja. Tukipendana, Mungu akaa ndani yetu, na mapendo yake yametimilika ndani yetu. Katika hili twatambua ya kuwa twakaa ndani yake, naye ndani yetu: kwa kuwa ametugawia Roho yake. Nasi tumeona na kushuhudia ya kuwa Baba amemtuma Mwanae awe Mwokozi wa dunia. Mtu akiungama kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, Mungu akaa ndani yake huyo, na yeye ndani ya Mungu. Nasi tumeyatambua na kuyaamini mapendo, Mungu aliyo nayo kwetu sisi. Mungu ni mapendo. Naye anayekaa katika mapendo, akaa ndani ya Mungu, naye Mungu akaa ndani yake. Katika hili mapendo yametimilika ndani yetu, ili tuwe na tumaini sabiti siku ile ya hukumu: kwa kuwa ginsi Yesu alivyo, nasi tulivyo hapa duniani. Katika mapendo hakuna hofu; lakini mapendo matimilifu hufukuza hofu, kwani hofu yaelekea azabu, naye mwenye hofu hakutimilika katika mapendo. Sisi tunapenda kwa sababu Mungu ametupenda  Yeye wa kwanza. Mtu akisema ya kwamba “nampenda Mungu”, naye anamchukia nduguye, ni mwongo. Maana asiyempenda ndugu yake anayemwona, hawezi kumpenda Mungu asiyemwona. Hii ni amri tuliyopokea kwake: ya kwamba ampendaye Mungu, ampende na ndugu yake.

*1 Yoane 4,16.7*

*R/* Nasi tumeyatambua mapendo, Mungu aliyo nayo kwetu sisi,  * naye anayekaa katika Mapendo, akaa ndani ya Mungu, naye Mungu akaa ndani yake.

*V/* Tupendane kwani mapendo yatoka kwa Mungu,  * naye anayekaa …

SOMO LA PILI

*Somo hili limetuwaliwa katika hotuba ya BONIFACIA RODRIGUEZ CASTRO, aliyeanzisha Jamaa yetu ya “Watumishi wa Mtakatifu Yusufu”, siku ya nne Takatifu, katika shirika la Salamanque.*

## Kumfuata Yesu

Mabikira wapenzi,

Kama sisi hatufuati nyayo za Yesu, nani atamfuata? Yesu anapita akitafuta yule anayeteswa pamoya naye, anayempenda, anayemfuata. Ametuita kwa hiyo akitupatia wito wa bei kuliko mali zote za dunia.

Sisi tunapaswa kulinda muungano wa namna mbili, ikiwa tunapenda kuwa na heri hapa duniani na kujaliwa kwenda mbinguni: Muungano na Mungu katika ukimya, sala na fikara, mapendo ya sadaka, na tena umoja kati yetu katika mapendano, bila mapendeleo, kwa kuwa sisi wote tuko sawa mbele ya Mungu.

Kwa kubakia katika umoja na Mungu, hakuna jambo lenyi kufaa kuliko kubakia siku zote mbele yake. Mungu yuko mbele yangu, nami mbele yake; ananiona na kunipatia moyo. Kama hatutengani na wazo hiyo, kwa bidii tungeyafanya mambo yote! Tuanapata kwa wakati wote wema anaotujalia!

Nitawaambia wazi ya kama musitafute kusifiwa na kumbembelezwa. Musihangaike hata kidogo na hiyo, kwa sababu Mungu anawahangaikia. Tafuteni tu jinsi ya kuwa wema na mtapendwa na watu, watawapenda bila nyinyi kutafuta. Mabembelezi gani Yesu amepata? Zarau! Sifa gani walimtolea? Matusi na uzulumu! Nyinyi munataka yale Yesu hakuyataka?

Tena mbele ya kutenda, muangalie kwanza tabia ya wengine kuliko yenu! Munapaswa kuheshimu yale wengine wanataka kuliko yenu, sababu tunapaswa kuwa wote katika wote, katika kumfuata Yesu aliyesahau hali yake ya kuwa sawa na Mungu akijifanya mdogo kama watu kwa kutumikia bila kutumikiwa.

Wadada wapenzi, tusahau makosa tuliyotendeana kati yetu na tusiwe wagumu kwa kuhurumia. Tujifunze kwa Yesu, hasa katika mateso yake. Mfano gani anatupatia! Sababu gani tukimwona kuteswa katika ukimya, hatuwezi sisi pia kulinda ukimya huu bora!

Wakati Enjili inatuhadisia jinsi walimchongea Bwana wetu, inatuambia kama Yesu amebaki kimya. Alinyamaza kwa kutufundisha kunyamaza.

Kusiwe masimango, malalamiko ao mazungumuzo ya siri, kwa sababu moto huu unaweza kuunguza nyumba yetu. Tujikaze kuleta mifano mizuri itakayotusaidia kuliko fikara na usomi wowote.

Wadada wapenzi, tupeane mifano na mimi mitaanza, nikiwahaidia mbele ya Mungu, na nyinyi ni mashahidi wangu.

*KIITIKIO Wafilipi 2,5.3.2*

K/ Muwe kati yenu na mawazo yale aliyokuwa nayo Kristu Yesu.
Muwaangalie wengine kama kuwapita nyinyi wenyewe.
* Musifanye kitu katika roho ya ushindani ao ya sifa za bure.

W/ Muwe na mapendo mamoja, moyo mmoja, mawazo mamoja.
* Musifanye kitu katika roho ya ushindani ao ya sifa za bure.

*SALA kama sala ya asubui*
*TE DEUM*

## 3. SALA YA ASUBUI

*WIMBO*

*ZABURI 62 Hamu ya Mungu*

*Ant. 1* Ni vema, ee Bwana, kuungana nawe na kutembea mbele ya uso wako.
*(W.P.:* Aleluya)

Ee Mungu, Mungu wangu, ninakutafuta :
roho yangu inaona kiu kwako.
Mwili wangu unakutamani sana,
kama nchi kavu, yenyi kiu, isiyo na maji.

Hivyo nilikutazamia hakaluni,
nione ezi yako na utukufu wako.
Neema yako ni bora kuliko uzima,
kwa hiyo midomo yangu ilikutukuza.

Nitakusifu katika maisha yangu,
kwa jina lako nitainua mikono yangu.

Roho yangu itashiba kama kwa mafuta,
kinywa changu kitakusifu kwa shangwe midomoni.

Ninapokukumbuka kitandani pangu,
wakati wa makesha ninakufikiri Wewe.
Kwa maana umekuwa msaada wangu,
na kivulini mwa mabawa yako nashangilia.
Roho yangu inaambatana nawe,
mkono wako wa kuume unanitegemeza.

Wanaojaribu kupoteza uzima wangu,
watumbukie mashimoni chini ya dunia!

Watolewe kuuawa kwa upanga,
wawe chakula cha bweha.
Lakini mfalme atamfurahia Mungu,
kila mtu anayeapa kwa yeye, atajisifu,
kinywa cha wawongo kitafungwa.

*Ant.* Ni vema, ee Bwana, kuungana nawe na kutembea mbele ya uso wako.
*(W.P.:* Aleluia)
*Ant. 2* Ninyi watakatifu na wanyenyekevu moyoni, mumtukuze Bwana.
*(W.P.:* Aleluia)

*WIMBO wa Danieli Dan. 3,57-88.56*
*Wimbo wa ulimwengu.*

Enyi nyote, viumbe vya Bwana, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi nyote malaika wa Bwana, mkuzeni Bwana!
Msifuni na kumwazimisha milele!
Enyi mbingu za Bwana, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi maji ya juu ya anga, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi mawezo yote ya Bwana, mkuzeni Bwana,

kwake utukufu mkuu ya sifa milele!
Enyi jua na mwezi, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi nyota za mbinguni, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi nyote mvua na manyungu, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi nyote pepo, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi moto na hari, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!

Enyi kipwa na masika, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi umande na sakitu, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi gandamizi na baridi, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi barafu na seluji, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi usiku na mchana, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi mwanga na giza, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi umeme na mawingu, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Nchi yote imkuze Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi milima na vilima, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi mimea yote mchipukayo katika nchi, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi chemchemi, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi bahari na mito, mkuzeni Bwana,

kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi nyangumi na vyote vitembeavyo majini, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi nyote ndege za angani, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi nyote wanyama wa porini na mifugo, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi wanadamu, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Ewe nyumba ya Israeli, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!

Enyi makuhani, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi watumishi wake, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi mioyo na roho za watu wema, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Enyi watakatifu na wanyenyekevu wa moyo, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!
Hanania, Azaria, Mishaeli, mkuzeni Bwana,
kwake utukufu mkuu na sifa milele!

*Ant. .* Ninyi watakatifu na wanyenyekevu moyoni, mumtukuze Bwana.
*(W.P.:* Aleluya)
*Ant. 3* Bwana anapenda taifa lake na kuwapa ushindi wanyenyekevu.
*(W.P.:* Aleluya)

*ZABURI 149 Furaha ya Watakatifu.*

Mwimbieni Bwana wimbo mpya;
sifa yake ivume katika mkutano wa waamini.
Israeli amfurahie Mwumbaji wake,
wana wa Sioni wamshangilie Mfalme wao.

Wasifu jina lake kwa michezo,
wamwimbie kwa ngoma na kinubi.
Kwa kuwa Bwana apendezwa na taifa lake,
awapamba wanyonge wokovu.

Waamini washangilie kwa utukufu,
waimbie kwa furaha vitandani.
Sifa za Mungu ziwe kooni mwao,
na upanga wenye makali kuwili mikononi mwao:
ili wawalipe mataifa kisasi,
na kabila za watu azabu;

ili wawafunge wafalme wao kwa minyororo,
na wakuu wao mapingu ya chuma;
ili wawafanyie hukumu iliyoabdikwa,
ndiyo sifa ya waamini wake wote.

*Ant.* Bwana anapenda taifa lake na kuwapa ushindi wanyenyekevu.
*(W.P.:* Aleluya)

*SOMO FUPI Yeremia 17,7-8*

Heri mtu anayemwaminia Bwana,
aliyeweka matumaini yake katika Bwana.
Atakuwa kama myi uliopandwa kando ya maji,
uenezao mizizi yake penyi mto:
wala hauogopi wakati wa hari unapofika,
nayo majani yake yazidi kuwa mabichi;
wala hauhangaiki katika mwaka wa ukavu,
wala hauachi kuzaa matunda.

*KIITIKIO*

*V/* Bwana anamsaidia * asubui na mapema.
*R/* Mungu akiwa karibu naye, hawezi kuwa mzaifu * asubui na mapema.

Sifa kwa Baba …

*Wakati wa Paska*

*V/* Bwana anamsaidia asubui na mapema * Aleluya, Aleluya.
*R/* Mungu akiwa karibu naye, hawezi kuwa mzaifu * Aleluya, Aleluya.
Sifa kwa Baba …

*ATUKUZWE BWANA Lk. 1,68-79*

*Ant.* Sawa Yesu, mfanya kazi pale Nazareti, Bonifacia anaungana na Mungu
Katika kazi zake za kila siku. *(W.P.:* Aleluya)

Atukuzwe Bwana, Mungu wa Israeli,
kwani ameangalia taifa lake na kulikomboa.
Ametuamshia Mwokozi mwenye nguvu,
katika nyumba ya Davidi, mtumishi wake.
Kama alivyosema zamani za kale
kwa kinywa cha manabii wake watakatifu.
Ili atuopoe katika adui zetu
na katika mikono ya wote wanaotuchukia.
Hivyo amewatendea baba zetu kwa wema,
hivyo amekumbuka agano lake takatifu,
maana alimwapia Abrahamu, baba yetu,
kama atatupatia sisi:
tuokoke katika mikono ya adui zetu,
ili bila hofu tumtolee ibada,
kwa utakatifu na unyofu
mbele yake siku zote za maisha yetu.
Nawe, mtoto, utaitwa nabii wa Yule Aliye-juu,
kwani utamtangulia Bwana kutengeneza njia zake ;
kuwajulisha watu wa taifa lake wokovu,
kwa maondoleo ya zambi zao ;
kwa ajili ya moyo mwema wa Mungu wetu,
aliyetuangalia sisi kama jua kipandalo juu
ili awaangazie wale wanaokaa katika giza na kivuli cha kifo,

na kuongoza miguu yetu katika njia ya amani.

*Ant.* Sawa Yesu, mfanya kazi pale Nazareti, Bonifacia anaungana na Mungu katika kazi zake za kila siku. *(W.P. :* Aleluya)

*MAOMBI*

- Tumshukuru Bwana kwa furaha, yeye aliyemwita Mtakatifu Bonifacia aendeleshe maisha ya Yesu, mfanya kazi pa Nazareti, katika Eklezya, na tuseme: tunakushukuru Bwana na tunaweka tumaini letu kwako.
- Aksanti Bwana Yesu, kwa sababu ulipokuwa pa Nazareti na kutumika pamoja na Yosefu na Maria, ulitufundisha kujitakatifuza kwa kazi na unyenyekevu.

- Ee Bwana Yesu, pamoja na Baba yako, unaendelea kufanya kazi kwa ajili ya dunia, utusaidie kwa mfano wako, tuendeleshe kazi ya Mungu ya kuumba dunia katika kazi zetu za kila siku.
- Ulimwita Mtakatifu Bonifacia awe mwanga katika kazi za watu duniani, utusaidie nasi tutumie vizuri zawadi hiyo kwa faida ya ndugu zetu.
- Ee Yesu, Baba alikutuma uwahuburi maskini Habari Njema, utusaidie kufuata nyayo zako, kama vile Mtakatifu Bonifacia, tutambue kama ni lazima tuwasaidie wawe watu kweli na tuendelee kuwaonyesha wokovu wako.
- Tunakushukuru Baba, Bwana wa mbingu na dunia, kwani ulificha mambo hayo kwa wenye elimu na wenye akili, ukayajulisha kwa wadogo.

Baba yetu …

*SALA ya mwisho*

Mungu Baba yetu, ulimwita Mtakatifu Bonifacia, bikira, amfuate Mwana wako katika ukimya na awatumikie maskini katika sala na kazi; utujalie kama yeye, tutafute Ufalme wako kuliko vyote hapa duniani na kusharikia mema ya milele ndani ya nyumba yako. Kwa ajili ya Kristu Bwana wetu. Amina.

## 4. SALA YA MANGARIBI

*WIMBO*

*Ant. 1* Wanaishi katika usalama wale wanaompenda Mungu. *(W.P.:* Aleluya)

*ZABURI 121*

Nalifurahi waliponiambia:
"Twende nyumbani kwa Bwana!"

Sasa miguu yetu imesimama
milangoni pako, ee Yerusalemu.

Yerusalemu uliojengwa kama mji
wenye kuungamana wote.

Ndiko wanakopanda makabila,
makabila ya Bwana,
kama ilivyo sheria ya Israeli,
ili watukuze jina la Bwana.
Humo vimewekwa viti vya hukumu,
viti vya nyumba ya Daudi.

Ombeni amani kwa Yerusalemu:
"Wenyi kukupenda wawe salama.
Amani iwe ndani ya kuta zako,
salama ndani ya majumba yako!"

Kwa ajili ya ndugu zangu na wenzi wangu,
nitasema: "Amani kwako!"
Kwa ajili ya Nyumba ya Bwana, Mungu wetu,
nitakuombea heri.

*Ant.* Wanaishi katika usalama wale wanaompenda Mungu. *(W.P.:* Aleluya)

*Ant. 2* Bwana anaongoza matendo ya mikono yetu. *(W.P.:* Aleluya)

*ZABURI 126*

Bwana asipojenga nyumba,
wanaoijenga wanasumbuka bure.
Bwana asipolinda mji,
mlinzi anakesha bure.

Ni bure kwenu kuamka asubui na mapema,
na kukesha mpaka usiku sana,
na kula mkate wa taabu!
Yeye amjalia mpenzi wake katika usigizi.

Tazama, unaopewa na Bwana ni wana,
tuzo lake ni mazao ya mwili.
Kama mishale mkononi mwa mpiga vita
ndivyo walivyo wana wa ujana.
Heri mtu aliyejaza podo lake nao,
hatahangaika anaposhindana na adui mlangoni.

*Ant.* Bwana anaongoza matendo ya mikono yetu. *(W.P.:* Aleluya)

*Ant. 3* Tokea utimilifu wake, sisi wote tumepewa neema na neema tena. *(W.P.:* Aleluya)

*WIMBO Waefeso 1,3-10*

Atukuzwe Mungu
Baba wa Bwana wetu Yesu Kristu,
aliyetubariki mbinguni katika Kristu,
kwa baraka yoyote rohoni.

Kwani ametuchagua ndani yake Yeye,
ulimwengu alipokuwa haujasimikwa bado
ili tuwe watakatifu na watu wasio na kosa
mbele ya macho yake.

Kwa mapendo yake
ametuweka tangu mwanzo
tupokelewe naye kuwa wana wake
kwa njia ya Yesu Kristu, na ndani yake.

Amekusudia hivyo
katika mapenzi yake mema,
apate kusifiwa utukufu wa neema yake,
aliyotujalia katika Mwana wake mpenzi.

Katika damu yake huyo
tumepewa ukombozi,
na maondoleo ya makosa yetu,
kadiri ya wingi wa neema yake.

Mungu amezidisha ndani yetu neema hiyo,
inayotuletea hekima na ufahamu wote
maana ametujulisha Fumbo la wokovu,
alilokusudia katika mapenzi yake mema.

Katika Mwana wake
ameweka tangu mwanzo Fumbo hilo,
apate kulitimiza nyakati zinapotimia:
kukusanya vyote chini ya kichwa kimoja,
ndiye Kristu,
vyote vya mbinguni na vyote vya duniani.

*Ant.* Tokea utimilifu wake sisi wote tumepewa neema na neema tena. *(W.P.:* Aleluya)

*NENO LA MUNGU  1 Wakorinto 1,27-30*

Lakini Mungu alichagua walio wapumbavu machoni pa dunia, ili awatie haya walio na hekima; na walio zaifu machoni pa dunia Mungu amewachagua, ili awatie haya walio na nguvu; na walio na asili nyonge machoni pa dunia na wenye kuzarauliwa Mungu amewachagua; ndio wote wasio kitu, ili awaangamize walio kitu: kusudi mtu hata mmoja

asijivune mbele ya Mungu. Kwa neema yake Yeye, ninyi mmepata kuwapo katika Kristu Yesu, aliyefanywa hekima kwetu kutoka kwa Mungu, na unyofu na utakatifu na ukombozi.

*KIITIKIO*

*R/* Ee Bwana, moyo wangu hauna kiburi * wala macho yangu hayainuki.
*V/* Wala sikufuata mambo makubwa yanayonipita * wala macho yangu hayainuki.
Sifa kwa Baba …

*Wakati wa Paska*

*R/* Ee Bwana, moyo wangu hauna kiburi, wala macho yangu hayainuki. * Aleluya, Aleluya.
*V/* Wala sikufuata mambo makubwa yanayonipita, wala macho yangu hayainuki. * Aleluya…
Sifa kwa Baba …

*WIMBO wa Maria Lk. 1,47-55*

*Ant.* Yesu anamtafuta yule anayekubali kuteswa naye, kumpenda na kumfuata.
*(W.P.:* Aleluya)

Moyo wangu unamtukuza Bwana,
na roho yangu inamshangilia Mungu, mwokozi wangu!
Maana ameangalia udogo wa mtumishi wake,
kweli tangu leo vizazi vyote vitanitaja mwenye heri.
Kwani Mwenyezi amenitendea makuu:
Jina lake ni takatifu.
Wema wake umeenea vizazi kwa vizazi,
kwa watu wenye kumheshimu.
Ametenda nguvu kwa mkono wake,
amewatawanya wenyi kujivuna moyoni.
Amewaangusha wakubwa chini ya viti vya ezi,
amewapandisha wadogo.
Wenye njaa amewajaza mali;
wenyi mali amewaondosha mikono mitupu.
Amemshurulikia Israeli mtumishi wake,

akikumbuka wema na ahadi zake,
alizozitoa kwa baba zetu,
Abrahamu na wazao wake kwa milele.

*Ant.* Yesu anamtafuta yule anayekubali kuteswa naye, kumpenda na kumfuata.
*(W.P.:* Aleluia)

*MAOMBI*

Tushangilie sikuu kuu ya Mtakatifu Bonifacia na tumshukuru Mungu Baba kwa sababu aliangalia udogo wake na tusali:

- Tunakushukuru, ee Baba, kwani ulitubarikia katika Kristu na neema tele yenyi kutoka mbinguni.
- Tunakushukuru kwani Mtakatifu Bonifacia alichagua njia ya mapendo inayounganisha katika umoja kweli.
- Tuishi katika ukimya na tusahau makosa yale tuliyotendeana sawa yeye na tusishindwe kuhurumiana, tupate nasi kuhurumiwa makosa yetu
- Mapendano yanaonyesha kama tunakuwa wafuasi wako, ee Bwana, kwani ndiyo mapenzi yako na hivyo Eklezya itaonyesha wazi sura ya mapendo ya Mungu Baba.
- Tunakuomba, ee Baba, ulivyomfufua Mwana wako, uwafufue pia wale waliofariki, wapate kuungana milele na mapendo na wema wako.

Baba yetu …

*SALA*

Mungu Baba yetu, ulimwita Mtakatifu Bonifacia, bikira, amfuate Mwana wako katika ukimya na kuwatumikia maskini katika sala na kazi; utujalie kama yeye, tutafute Ufalme wako kuliko vitu vyote hapa duniani na kusharikia mema ya milele ndani ya nyumba yako.
Kwa ajili ya Kristu, Bwana wetu.